Toleo 67 - Muharram 1444 AH / Agosti 2022 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Tunawapongeza Kwa Munasaba Wa Eid Ul –Adh-Ha

**HABARI NA MAONI**
Uchaguzi Wa Agosti 9: Zoezi Lisilokuwa Na Maana

**MATOLEO**
Uhalisia Wa Chaguzi Za Kidemokrasia Na Hukumu Ya Kiislamu Juu Yake

**JIBU LA SWALI**
Je, Bismillahi ni Sehemu ya Suratul Faatiha?



# CHAGUZI ZA KIDEMOKRASIA NI SARABI, HUDHANIWA NI MAJI KWA MWENYE KIU

uqab.or.ke uqab_htk UQABMagazine

Afisi kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 10/1443 Alhamisi, 17 Dhul-Hijjah 1443 H 10/07/2022 M

Taarifa kwa Vyombo Vya Habari

# Tunawapongeza Kwa Munasaba Wa Eid Ul –Adh-Ha

Harakati ya Hizb ut-Tahrir Kenya ingependa kutuma salamu za dhati za Id ul-Adha kwa Waislamu humu nchini na wote dunia kwa ujumla. Tunatuma salamu zetu wanaume na wanawake wanaofanyakazi kwa juhudi kubwa katika kusimamisha tena Khilafa ya Pili kwa mfumo wa utume. Kama vilevile tungependa kumtumia salamu zetu Amiri wa Hizb ut-Tahrir Mwanachuoni mkubwa Ataa Bin Khalili Abu al-Rashta kwa munasaba wa kuingiliwa na Idul –Adha.

Idi hii tukufu inakuja huku kiwango cha mfumoko wa bei kimefikia hadi asilimia 7.9 hali iliopelekea bei ya vyakula kupanda maradufu.Kinaya ni kuwa huku raia wakiumizwa na hali hii wanasiasa wa mirengo yote wamejikita katika kuhadaa raia kwenye kampeni za uchaguzi wa Agosti 9 kwamba eti maendeleo ni kutia kura debeni. Mfumoko ni janga la kutengezwa chini ya mfumo wa Kibepari na utaratibu wake pesa za makaratasi. Kwa kuwa Mfumo wa Kirasilimali na itikadi yake ya Kiilmaania imekataa mfumo utokao kwa Mwenyezi Mungu SWT nao ni Uislamu hivyo maisha ya wanadamu yapo kwenye dhiki.

Tunaposherehekea Idi hii, twapasa kujikumbusha mtihani mkubwa aliokumbana nao nabii Ibrahim (as) na jinsi alivyokuwa tayari kujitolea. Leo walinganizi wa Khilafah wanapata mateso ya tawala za kidhulma kote duniani. Kwa hakika tupo katika kipindi cha kujitolea cha kuulingania Uislamu kama mfumo mbadala wa Mfumo uliofeli wa Kirasilimali na hapo ndio suluhisho litapatikana kwa matatizo ya ulimwengu na kuwa na tija kubwa.

Mwisho twamuomba MwenyeziMungu SWT kutakabali amali zetu njema na atuongoze hadi kufikia Idi nyengine tukiwa ndani ya kivuli cha Khilafah Raashida kwa mfumo wa Utume itakayo unganisha Waislamu wote duniani chini ya bendera ya Laa ilaha ila Ilah Muhammad Rasul Allah.

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari**
**Hizb ut-Tahrir Kenya.**

# Uhalisia Wa Chaguzi Za Kidemokrasia Na Hukumu Ya Kiislamu Juu Yake.

Huku ikiwa zimesalia siku chache kabla ya uchaguzi mkuu hapo Agosti 9 chini ya kibandiko cha mageuzi, wanasiasa wanazunguka kona zote za nchi kutaka kupigiwa kura. Mazungumzo ya raia wa kawaida ambao wengi wao masikini hawajui uhalisia wa siasa ya kidemokrasia na wanasiasa wake nao wapo katika mazungumzo mikahawani, vijiweni na maskani wakishindana nani atashinda hasa kwenye kura za urais! Bila shaka pesa zinaangamizwa kwenye kampeni hizi ambazo zimejaa kila aina ya vitisho, urongo,chuki na matusi. La kutia machungu zaidi ni Waislamu kushughulika na uchaguzi huu kana kwamba ndio kadhia yao nyeti hapa duniani! Mashekh na Maustadh hutoa fatwa za kuhimiza watu kushiriki kwenye chaguzi za Kidemokrasa wakitumia Aya na Hadithi!

Kwenye Makala yangu haya sitaki kuingia katika fatawa hizi za masheikh bali napenda niweke msitari kati ya haki na batil na halali na haramu. Ili kujua hukumu ya kisheria katika suala la uchaguzi wa Kidemokrasia awali ya yote ni muhimu kubaini kile wana usuli hukiita tahqiq –manat (uhalisia na uhakika wa maana) ya chaguzi za kidemokrasia. Yaani hapa hatuna budi kueleza nini maana ya uchaguzi na nini maana Demokrasia kisha baadae ndio tututoe hukmu ya Kiislamu juu yake.

Uchaguzi ni uwakala yaani mtu kuchagua mtu mwengine amfanyie kitendo kwa niaba yake. Kwa mfano Msikitini twaeza tukatangaza nafasi za uimamu.Wakajitokeza watu watatu au wane wenye sifa za uimamu na hapa twataka imamu mmoja tu, hivyo maratibu wakachagua kati ya wanne hawa mmoja wao kwa kupitia kura.

**Nabii Yunus AS :** Kulipigwa ndani ya jahazi lililizidiwa na uzito ikabidi ipigwe kura na yule atakayeangukiwa na kura basi atoswe bahari. Yunus AS ikamwangukia yeye na akatoswa baharini.

فَسَاهَمَ فَكَانَ مِنَ ٱلْمُدْحَضِينَ

[Swafat: 141]

**Kwa Nabii Zakaria AS:** Katika kutafuta nani amlee Nana Maryam basi kura ikatumika

ذَلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهِ إِلَيْكَ وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ يُلْقُونَ أَقْلَامَهُمْ أَيُّهُمْ يَكْفُلُ مَرْيَمَ

**Hizi ni khabari za ghaibu tunazokufunulia nawe hukuwa nao walipokuwa wakituma kalamu zao ndani ya Maji(kwa kura) wajue nani katika wao watamlea Maryam. [Al-Imran:44]**

**Mtumi Muhammad SAAW:** Amepokea Imam Bukhari kutoka kwa Nana Aisha RA

كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا أَرَادَ سَفَرًا أَقْرَعَ بَيْنَ نِسَائِهِ ، فَأَيَّتُهُنَّ ” خَرَجَ سَهْمُهَا خَرَجَ بِهَا مَعَهُ ،

**Mtume SAW alipotaka kusafiri basi alikuwa akipiga kura baina ya wakeze na yule aliekuwa ikimwangukia basi ndiye aliekuwa akitoka naye.**

Tuje katika maana ya chaguzi katika Demokrasia. Ni muhimu kufahamu kwamba Demokrasia ni mfumo wa kiutawala wala sio kupiga kura. Demokrasia asili ni matamshi mawili yenye asili ya Kigriki Demos ambao humaanisha watu na cratos ikimaanisha utawala kwa maana ni utawala wa watu. Utawala huu humaanisha wanadamu wanamiliki ubwana (sovereignity) unaowawajibisha watunge kanuni ambazo ndio hutukuzwa kuliko sheria za Mwenyezi Mungu(swt). Hivyo Bunge au baraza la seneti, la wawakilishi au Congress zote katika demokrasia ni taasisi za kutunga kanuni. Sasa Demokrasia huchukua mbinu ya uchaguzi kila baada ya miaka 5 au 4 ya watu kuwachagua watu wawe ni wawakilishi wao katika kazi ya kutunga kanuni. Kwa kifupi chaguzi za Kidemokrasia zinafungika katika kitendo cha kutunga sheria ambacho ni kinyume na Uislamu.

Kwa mujibu wa Uislamu, sheria ni miliki ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kumaanisha kwamba Wanadamu haki yao sio kutunga sheria bali ni kufuata sheria za Mwenyezi Mungu (s.w.t). Mwanadamu hafai kabisa kutunga sheria hata kama imeambatana na sheria ya Mwenyezi Mungu(s.w.t) kwani kinachokatazwa ni kitendo cha kutunga sheria. Bali Uislamu umewajibisha kufuata sheria za Mwenyezi Mungu (s.w.t). Asema Allah swt:

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُواْ فِىٓ أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُواْ تَسْلِيمًا

**Naapa na Mola wako mlezi hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitilafiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenyekee kabisa. [An-Nisai: 65]**

Huu ndio uhalisia wa uchaguzi hivyo kinachofanya uchaguzi usemwe ni haramu au halali si uchaguzi kwa dhati yake bali ni kile kitendo ambacho kinafungika na ule uchaguzi wenyewe. Kwa haya chaguzi za kidemokrasia zinakiuka misingi ya Kiislamu hivyo ni batili kisheria, na haramu kwa Waislamu kuunga mkono vyama vya kidemokrasia na kushiriki ndani yake.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari**
**Hizb ut Tahrir Kenya**

 **Email: info@uqab.or.ke**

# CHAGUZI ZA KIDEMOKRASIA NI SARABI, HUDHANIWA NI MAJI KWA MWENYE KIU

Agosti 9 ni siku ya uchaguzi nchini Kenya utakaokuwa wa sita wa vyama vingi tangu kurudishwa tena Demokrasia ya vyama vingi mwaka 1992. Vyama 82 vitashiriki katika uchaguzi huu, kando na wagombea watakao simama bila ya vyama. Walioonesha azma ya kuwania urais ni 47 ila 4 tu ndio walioweza kuidhinishwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC). Kati ya hao ni Raila Odinga wa ODM (Muungano wa Azimio) au William Ruto wa UDA (Muungano wa Kenya Kwanza) ndio walio na tamaa ya kushinda uchaguzi huu. Kama ilivyo ada miungano hii imejipanga kikabila na cheche zake zimedhihirika mapema katika kampeni kiasi ya kutia hofu wadadisi wa kindani na wale wa kimataifa juu ya usalama wa nchi wakati wa uchaguzi na baada yake.

Uchaguzi huu utafanyika wakati wananchi wapo katika hali ya mfadhaiko haswa upande wa kiuchumi na kiusalama ingawa hali hii ngumu imekuwa ikizidi miaka hadi miaka. Hali hizi mbili, zimefikia hali mbaya wala hakuna tamaa ya kutatulika kwa uharaka ila imekuwa ni ajenda iliyodandiwa na wagombea urais kwa malengo ya kuwavutia wapiga kura. Upande wa kiuchumi kila mwaka wa uchaguzi kuna dhihirika mdororo kwa kiasi kikubwa zaidi kuliko miaka mingine isiyokuwa ya uchaguzi. Ukuaji wa uchumi ulishuka katika miaka ya uchaguzi wa mwaka 2002, 2007, 2012, 2017 kwa asilimia 0.2, 0.5, 3.8 na 3.8 mtawalia na yatarajiwa mwaka huu itashuka zaidi. Miongoni mwa mambo yanayochangia kudorora kwa uchumi ni pamoja na:

Kwanza- Mfumuko wa bei ambao umezifanya bidhaa muhimu ikiwemo chakula hususan mahindi kufikia kiwango cha Ksh250 kwa mfuko wa kilo 2.

Pili- Mgogoro wa kivita baina ya Urusi na Ukraine umesababisha upungufu wa ngano na mbolea nchini, kwa kuwa Kenya inaagiza asilimia 90 ya ngano na mbolea kutoka nchi hizo mbili!

Tatu- Makampuni, wafanyibiashara na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wameingiwa na wasiwasi kutokana na hatima ya uchaguzi huu. Huku sababu hizi zikitajwa na wanasiasa kuwa ndio chanzo cha hali ngumu ya maisha hivi sasa, ukweli unabakia kuwa ni mfumo wa kiuchumi wa kibepari ambao asili unajali maslahi ya tabaka la mabwenyenye wanaomiliki uzalishaji na usambazaji wa rasilimali. Kwa uhakika kila mwenye kufikiria kwa kina atafahamu kwamba mfumko wa bei umekuweko hata kabla ya vita huko Ukraine! Hata hivyo, hofu hiyo imekitwa katika msingi wa mvutano wa walionacho 'dynasties' na wasiokuwa nacho 'hustlers' na imepelekea mzunguko wa pesa kupungua kwa kiasi kikubwa sokoni na hata kupunguza hifadhi ya sarafu za kigeni katika Benki Kuu hususan Dola ya Amerika.

Ama upande wa kiusalama, tayari raia wameanza kuhisi tishio juu ya maisha yao hususan kutokana na matamshi ya uchochezi kutoka kwa wanasiasa. Miongoni mwa matamshi hayo ni 'hatutaki madoadoa, kama ni noma iwe noma.' Matamshi hayo pamoja na kuibuka kwa vikundi na magenge yanayodaiwa kudhaminiwa na kutumiwa na wanasiasa ili kuwahangaisha na kuwashambulia wapinzani wa kisiasa pamoja na wafuasia wao. Kwa kuongezea, Kenya hivi sasa inakodelea janga la kielimu kutokana na kuharakishwa utekelezaji wa mtaala mpya wa elimu maarufu CBC kwa kuwa miundo mbinu na rasilimali msingi hazijawa tayari na hivyo kuhatarisha maisha na mustakbali wa watoto zaidi ya milioni 1.4 wanaotakiwa kujiunga na JSS.

Enyi Waislamu, Wanasiasa pamoja na manifesto zao zote wamefaulu kuhadaa raia kuamini kubwa matatizo yanayowakabili yatatuliwa kupitia uchaguzi. Cha ajabu chaguzi tano zimepita ilhali matatizo huzidi bali ni wazi kuwa manifesto hizi hubakia kwa maandishi tu pasina na kutekelezwa na ushahidi wa haya uko wazi kabisa.

Hakika, chaguzi za kidemokrasia ni sarabi (mazigazi) kwa mwenye kiu hudhaniwa ni maji ilhali sio. Kwa kuwa vyama vyote vya kisiasa na ilani zao zimetenga Uislamu mbali hakuna lolote litakaldhaminia suluhisho la kweli. Chaguzi hizi kiasili hutumika katika kuhalalisha zoezi la upigaji kura na sio kuwa ndio chanzo cha kusuluhisha matatizo kimsingi. Kwa mfano wagombeaji wa urais wanaahidi mengi. Ruto ameahidi kushukisha rasilimali mashinani ili kuwanyanyua walala hoi pamoja na kutenga bilioni Sh200 kwa ajili ya kutoa mikopo ya riba ya chini kwa wafanyibiashara wadogo. Huku Raila akiahidi kutoa Sh6,000 kwa mwezi kwa Wakenya milioni 8 wasiojiweza pamoja na elimu ya bure kutoka msingi hadi chuo kikuu! Hizo ni ahadi hewa hususan tukizingatia kuwa hali ya Kenya kiuchumi haiwezi kuhimili ahadi hizo kutokamana na madeni makubwa yaliyokopwa ndani na nje ya nchi ambayo sasa hivi yamefikia zaidi ya trilioni 8.2!

Hivyo basi, wakati umefika wa watu kufungua macho na kutambua kuwa chaguzi za kidemokrasia ni ndoto za mchana zilizojikita katika mchezo wa patapotea. Kwa kuwa wanasiasa wake hupatiliza dhiki za raia na kuwatumia kama ngazi ili kuingia madarakani. Kisha

***Endelea... UK 5***

kuwatupilia mbali na kutowajali hadi msimu ujao baada ya miaka 5. La msingi ni kufanya kazi usiku na mchana ili kurudisha tena maisha ya Kiislamu kwa ushirikiano na harakati ya Kiislamu ya Hizb ut Tahrir. Harakati isiyojali lawama wala ukosoaji kutoka kwa wapenzi wa demokrasia na mfumo wao wa kisekula wa kirasilimali. Ili kujitoa katika vitanzi au minyororo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kielimu hakuna budi kurudisha tena utawala wa Kiislamu wa serikali ya Khilafah katika nchi iliyotimiza vigezo na masharti yanayo zingatiwa.

وَٱلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ أَعۡمَٰلُهُمۡ كَسَرَابِۭ بِقِيعَةٖ يَحۡسَبُهُ ٱلظَّمۡـَٔانُ مَآءً حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءَهُۥ لَمۡ يَجِدۡهُ شَيۡـٔٗا

**“Na walio kufuru vitendo vyao ni kama sarabi (mazigazi) uwandani. Mwenye kiu huyadhania ni maji. Hata akiyaendea hapati chochote.” [24. An-Nur: 39]**

**Hizb ut-Tahrir Kenya**

**29/07/2022 M**

**30th Dhul Hijjah 1443 H**



# HABARI NA MAONI
## Uchaguzi Wa Agosti 9: Zoezi Lisilokuwa Na Maana




**Habari:**

Wakenya watashiriki uchaguzi mnamo 9 Agosti, 2022. Majirani wa Kenya wanafuatilia uchaguzi huu kwa umakini, kwa kuwa Kenya ndio kitovu cha kiuchumi cha Afrika Mashariki na Kati. Huu unatarajiwa kuwa uchaguzi wenye ushindani mkubwa baina ya muungano wa Kenya Kwanza unaoongozwa na Ruto na muungano wa Azimio unaoongozwa na Raila.

**Maoni:**

Kikatiba Kenya inatambuliwa kama nchi huru yenye ubwana, lakini kiuhalisia imebakia kuwa ni shamba la kikoloni. Kwa hiyo, walioko madarakani nchini Kenya wapo kwa ajili ya kudumisha na kuimarisha mahusiano ya kikoloni. Hivyo basi, siasa za kidemokrasia zina sifa ya kutoa ahadi nyingi na manifesto zinazovutia kama ngazi za kuwahadaa watu kwamba mustakbali wao ni mzuri. Hata hivyo, punde tu uongozi mpya unapoingia mamlakani, hutekeleza yale ambayo yanawafaidi wao, washirika wao na hususan maslahi ya mabwana zao wakoloni.

Kwa mara nyingine Wakenya wapo njia panda hawajui ima wapigie kura mgombea urais kutoka muungano wa Kenya Kwanza au Azimio. Kuwa njia panda huko kumetokana na kuwa wamemeza chambo hadaifu ambacho msingi wake ni siasa za kidemokrasia. Chambo hicho kinahusisha kushiriki uchaguzi kila baada ya muhula wa miaka mitano kwa msingi wa kuwa na matumaini juu ya sarabi 'wanasiasa' kwamba watatatua matatizo yao. Alas! Hakuna kinachotatuliwa na uchaguzi, badala yake ni kuwa mambo yanazidi kuwa magumu kila muda unaposonga licha ya kuwepo uongozi mpya.

Tangu uhuru bandia wa bendera mnamo 1963, Wakenya wanaendelea kutaabika kutokana na changamoto za kupindukia za kisiasa, kijamii na kiuchumi kama vile ukiritimba wa rasilimali za umma kwa kampuni za kigeni, umasikini na kipote cha wanasiasa waliochini ya ushawishi wa kimagharibi. Hakuna utawala tangu wakati huo umeweza kutatua changamoto zilizotajwa kwa sababu wao ni sehemu ya tatizo linalohitaji kutatuliwa kimsingi.

Suluhisho lipo katika kuondosha nidhamu ya uongozi wa kidemokrasia ambayo imelazimishwa juu ya shingo zetu na wakoloni wamagharibi. Nidhamu ambayo inatanua kwa kuendeleza mapengo na uchafu katika nyanja zote za maisha. Ni nidhamu ambayo imejikita na kupigia debe mchakato wa bahati nasibu katika usimamizi wa mambo ya watu. Ni kupitia kuiondosha PEKEE ndipo kutapatikana fursa kwa Wakenya, Afrika na ulimwengu hatimaye kuweza kupumua kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Kuiondosha na sehemu yake kuchukuliwa na nidhamu ya utawala wa Kiislamu ya Khilafah. Khilafah itapeana kipaumbele katika kusahilisha maisha ya watu na SIO kukazanisha vitanzi vya kisiasa, kijamii na kiuchumi, kama inavyofanyika hivi sasa nchini Kenya na ulimwenguni kote. Haishangazi kuona utawala unatumia uwezo wote ilio nao ili kuhakikisha kwamba masanduku ya kutilia karatasi za kupigia kura na karatasi zinafikishwa sehemu za ndani ndani kabisa. Lakini, tawala hizo hizo zinafeli katika kufikisha huduma msingi sehemu hizo hizo za ndani ndani!

Wasiwasi na hofu za kisiasa ziko juu kwa sababu nidhamu yenyewe ni natija ya vurugu za kisiasa baina ya watu wa kawaida na wanafikra wakiwa upande mmoja dhidi ya watawala 'wafalme' na makasisi huko Ulaya.

*Endelea... UK 7*


Email: info@uqab.or.ke

Ama nchini Kenya siasa za kidemokrasia zimejikita katika idadi na mirengo ya kikabila. Hivyo basi, Wakenya wanafuatilia kwa makini yale matamshi na maelekezo yanayotolewa na viongozi wao wa kisiasa.

Kushiriki katika uchaguzi kunadaiwa kuwa ni kutekeleza haki ya kidemokrasia, lakini kiukweli ni kuwa una halalisha ufisadi unaotekelezwa juu ya ardhi. Msingi wa ufisadi ni kuwatawala watu kwa kutumia tungo za akili na sio wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt). **إِنِ ٱلْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ "Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu."** [12. Yusuf: 40]. Hivyo basi, kila mzunguko wa uchaguzi tunawaona wanaojiita viongozi walewale wakitoa ahadi tupu lakini hakuna chochote kiuhalisia. Kwa kuongezea, lau watachangamkia mradi, lengo sio kuboresha maisha ya raia. Bali, lengo lao kuu ni kushiriki ili waweze kupata hongo kupitia miradi hewa na ubinafsishaji wa rasilimali za umma.

Kiuhakika, uchaguzi wa Agosti 9 sio chochote bali ni zoezi lisilokuwa na maana ambalo litaleta fujo na machungu zaidi kwa walioshiriki na ambao hawakushiriki. Historia ya uchaguzi wa kidemkorasia duniani inatoa taswira ya tawala zilizo sambaratika na wanadamu waliokata tamaa na waliozama katika simanzi. Mfano mzuri ni uchaguzi wa hivi majuzi wa Amerika ambao ulithibitisha kwa watu wote kwamba uchaguzi wa kidemokrasia ni mazoezi yasiyokuwa na maana na kwamba hakuna matumaini ya utulivu na ustawi kupitia kwayo. Amerika inayojiita kuwa ndio ngome ya demokrasia imethibitisha rasmi kwamba mungu wa demokrasia amefeli kabisa!

Kwa kutamatisha, hatutakiwi kupoteza muda katika bahati nasibu, badala yake tunatakiwa kuanza kufanyakazi kwa ajili ya kurudisha tena maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha Khilafah kwa njia ya Utume. **وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ ٱلْمُؤْمِنُونَ "Na siku hiyo Waumini watafurahi."** [30. Ar-Rum: 4].

Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI

# Manifesto Ya Vyama: Hali Ni Ileile Kamwe Haitobadilika Kwani Uislamu Umetupiliwa Mbali!

**Imeandikwa Kwa niaba ya Ofisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut-Tahrir Kenya**

**Habari:**

Mbio za kumsaka raisi wa serikali ijayo zimeshika kasi ikiwa tayari wagombea wa wadhifa wa urais, walioidhinishwa na tume ya usimamizi wa uchaguzi wakizindua rasmi manifesto zao kwa ajili yakupata kura za uchaguzi wa Mwezi Agosti 09. Raila Odinga anayewania kwa mara ya tano kiti cha urais, alizindua manifesto yake mapema mwa mwezi Juni ambayo kimsingi imejikita mabadiliko ya kiuchumi kwa kupitia uenezwaji wa viwanda. Akiahidi kuwa kila Gatuzi katika magatuzi yote 47 kuweko na kiwanda cha uzalishaji. Mpinzani wake wa karibu naib rais William Ruto ambaye kwake ni mara ya kwanza kugombea urais alizindua manifesto yake mnamo Juni 30. Manifesto yake nayo imejikita kwa misingi mitano ikiwemo: kufufua uchumi wa nchi kupunguza gharama za maisha, kuimarisha hali za vijana. Profesa Wajackoya ameteka masikizi takriban pembe zote za nchi pale ali[otaja kwenye manifesto yake kwamba atahalalisha bangi!

**Maoni:**

Manifesto za vyama vya kisiasa ni ada ya zamani ambapo huweka mkataba wake na wapiga kura. Kama zilivyokuwa manifesto za vyama vya kisiasa vya miaka ya nyuma, manifesto zilizozinduliwa hazina chochote kipya katika Aidilojia. Wanasiasa wa Kidemokrasia ama vyama wana hulka ya kutoa ahadi zisizo kuwa na sura wazi bali hujaza masuala ambayo serikali zote zilizopita hazikuweza kuzitekeleza. Kwa mfano utawala wa sasa unaondoka wa Jubilee kwenye manifesto yake uliahidi kubuni nafasi za kazi milioni 1.3 kila mwaka kwa vijana wasokuwa na kazi lakini wapi! ilikuwa ni ahadi tupu. Uhalisia wa mambo ni kwamba Kampeni za Demokrasia zinadhaminiwa na mabwenyenye mabepari wanaohonga wapiga kura kama chambo na kuwapata mawakala wa kisiasa ambao wakichaguliwa wafanye kila wawezavyo kulinda maslahi yao.

Kuhusu suala la uhalilishwaji wa bangi, hii inaonesha bayana jinsi itikadi ya Kisecular ilivyozalisha wanasiasa wanaotukuza maovu na fikra za kihuni. Kwa kutenganisha Dini na Maisha, usekula umesheheni wanasiasa wanaopelekwa na matamanio na wala sio sharia za MwenyeziMungu (Swt)

Yoyote atakayeshinda uchaguzi huu kwa hakika hatobadilishi kimsingi hali ngumu anayokabiliana nayo raia wakawaida. Hii ni kwa sababu uongozi katika Demokrasia ni urongo na tamaa tu ya kukidhi maslahi ya kibinafsi wala sio kujali maslahi ya watu. Serikali itakayoundwa itajifunga na sera unyonyaji za mfumo wa Kikoloni wa kirasilimali. Seuze ya hayo, hizi chaguzi za Kidemokrasia hufichua urongo na utapeli uliojikita kwenye kutoa ahadi tupu na kudai kwamba upigaji kura ndio njiya ya kufikia maendeleo na mabadiliko na mustakabali mwema.

Kwa kuwa manifesto zote hizi zimeweka Uislamu mbali katika ajenda ya mabadiliko, hii ina maanisha kuwa hali itabakii hiyohiyo wala haitobadilika.Uislamu una mengi ya kutekelezwa kikamilifu na una njia halisi ya kufikia mabadiliko ya kikweli ambao dunia nzima lazima ijukumike kuufanyia kazi.



Email: info@uqab.or.ke

**JIBU LA SWALI**

# Je, Bismillahi ni Sehemu ya Suratul Faatiha?



**Swali:**

Assalamu Alaikum Wa Rahmatullahi Wa Barakaatuh wa Maghfiratuh…

Namuomba Mwenyezi Mungu awaafikie kwa kila la kheri, kwani hakika yeye ni muweza wa hilo.

Swali langu ni: ikiwa wanazuoni wamekubaliana kwamba, yeyote anayepinga kuwa Bismillahi sio aya katika Al-Faatiha basi hawi kafiri. Kwa sababu (hiyo Bismillahi) imethubutu kwa njia ya Aahaad (kupokewa na watu wachache) na wala sio kwa njia ya Tawaatur (kupokewa na watu wengi sana)… sasa vipi iwe ni nambari katika baadhi ya misahafu mwanzoni mwa Al-Faatiha leo? Na lini iliingia kama aya katika Al-Faatiha? Na je, Al-Faatiha ni aya saba (7) ama sita (6) bila ya Bismillahi? Kwani misahafu imetafautiana katika kuhesabu nambari za Al-Faatiha. Na je, hili linapingana na hifadhi ya Mwenyezi Mungu kwa Qur`an tukufu? Na upi msimamo wa Dola ya Kiislamu ijayo in shaa Allah, juu ya uwepo wa vitu visivyokuwa mutawaatir kwenye msahafu, kama vile Bismillahi na dua iliyo mwishoni mwa msahafu?!

Na Mwenyezi Mungu awabariki.

**Jibu:**

Wa Alaikum Salaam Wa Rahmatullahi Wa Barakaatuh.

Tumeshatangulia kujibu swali kuhusiana na Bismillahi tarehe 21 Rabiul Akhir 1432 H – sawa na 11/3/2011 M. Na imekuja ndani yake haya yafuatayo:

[Kuhusu Bismillahi: ni aya katika Qur`an tukufu kama ilivyo kipande cha aya katika Surat al-Naml:

﴿إِنَّهُ مِنْ سُلَيْمَانَ وَإِنَّهُ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ﴾

**"Imetoka kwa Sulaiman nayo ni: Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu."** [Al-Naml: 30].

Ama katika mwanzo wa Al-Faatiha, au mwanzoni mwa sura (zengine) hili lina ikhtilaaf kwamba je, ni aya katika sura? Ama ni kipambanuzi tu kati ya sura (na sura nyingine)… na hii ikhtilaafu haidhuru, kwa sababu, pande zote mbili zinakubali kuwa (hiyo Bismillahi) ni katika Qur`an kwenye Surat al-Naml. Na ikhtilaafu ni kuhusu kuiweka mwanzo wa sura isiyokuwa Surat al-Tawba, je, (hiyo Bismillahi) ni aya pia mwanzoni mwa sura? Ama ni aya mwanzoni mwa Al-Faatiha? Ama sio aya mwanzo wa sura, wala mwanzo wa Al-Faatiha… Maadamu wote wanakubali kuwa (Bismillahi) ni aya katika Surat al-Naml, basi ikhtilaafu kuhusu kuwepo mwanzo wa sura haiathiri isipokuwa kwenye kuisoma katika swala mwanzo wa Al-Faatiha au mwanzoni mwa sura zengine, kusomwa kwa suati au kwa siri au kutoisoma kabisa, kulingana na hukmu za kisheria zilivyovuliwa na wanazuoni wenye kujitahidi] Mwisho wa nukuu.

*Endelea... UK 10*



Email: info@uqab.or.ke

Na ili kuzidi kuweka wazi zaidi na kujibu mambo mengine katika swali lako, nitataja mambo yafuatayo:

1- Imekuja kwenye kitabu cha “Shakhsiya” – Juzuu ya Kwanza – ukurasa wa 159 hadi 160 [Hakika Jibril alikuwa akisoma yote yaliyoteremshwa kwa Mtume (saw) katika Qur`an mara moja kila mwaka. Na katika ule mwaka ambao Mtume (saw) alikufa, Jibril alimsomea Mtume Qur`an yote mara mbili. Imepokewa kutoka kwa Aisha (ra) kutoka kwa Fatima (as) **“Mtume (saw) alinieleza kwa siri kwamba Jibril alikuwa akinisomea Qur`an yote kila mwaka mara moja, na hakika yeye amenisomea mwaka huu mara mbili, na sioni ila ni kwamba wakati wangu (wa kufa) umefika”** (imepokewa na Bukhari). Na imepokewa kutoka kwa Abu Huraira akisema: **“Alikuwa (Jibril) akimsomea Mtume (saw) Qur`an nzima kila mwaka mara moja, na akamsomea mara mbili kwenye mwaka ambao alikufa ndani yake”** (imepokewa na Bukhari).

Jibril kumsomea Mtume (saw) Qur`an kila mwaka mara moja, maana yake ni kumsomea kwa mpangilio wa aya zake kulingana na baadhi yake, na kwa mpangilio wa aya zake kwenye sura zake. Kwa sababu, kuaridhi kitabu maana yake ni kusoma ibara, matamshi, na mpangilio wake. Na Mtume kusomewa mara mbili katika ule mwaka aliokufa ndani yake, maana yake hivyo hivyo ni kusomewa kwa mpangilio wa aya zake kulingana na baadhi yake, na kupangilia aya zake ndani ya sura zake. Na pia yaweza kufahamika hivyo hivyo kutokana na hiyo hadithi kusoma kwa mpangilio wa sura zake kulingana na baadhi yake. Isipokuwa tu zimekuja hadithi zengine sahihi zikiwa wazi katika kupangilia aya, kwani zinaeleza wazi kupangilia aya kulingana na baadhi yake na kupangilia aya kwenye sura zake: «ضَعُوا هَذِهِ الآيَاتِ فِي سُورَةِ كَذَا بَعْدَ آيَةِ كَذَا» **“(Mtume akiwaambia) ziwekeni aya hizi kwenye sura kadhaa baada ya aya kadhaa”** «ضَعُوا هَؤُلَاءِ الْآيَاتِ فِي السُّورَةِ الَّتِي يُذْكَرُ فِيهَا كَذَا وَكَذَا» **“Ziwekeni aya hizi kwenye sura ambayo ndani yake kunatajwa kadhaa na kadhaa”**. Na ilikuwa sura hukamilika na kuanza nyengine kwa maelekezo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwa njia ya Jibril. Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas akisema: **“Mtume (saw) alikuwa hajui kumalizika kwa sura hadi inapoteremka Bismillahi ar-Rahmaani Ar-Rahiim”** na katika mapokezi mengine: **“Pindi inapoteremka Bismillahi ar-Rahmaani arRahiim ndipo wao hujua kuwa sura imemalizika”** (Sunan al-Baihaqi na Abu Dawud). Yote hayo yanajulisha kwa kukatikiwa kwamba, mpangilio wa aya katika sura zake, na muundo wa sura kwa idadi ya aya zake na maweko yake, yote hayo yalikuwa kwa maelekezo yatokayo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na hivyo ndivyo Umma ulivyopokea kutoka kwa Mtume wao (saw), na hayo yakathubutu kwa njia ya Tawaatur (mapokezi ya watu wengi kutoka kwa wengi …]

2- Na wakati maswahaba (ra) walipotegemea msahafu wa Uthmaan walithibitisha ndani yake Bismillahi mwanzoni mwa Al-Faatiha na mwanzoni mwa sura zengine isipokuwa Surah al-Baraa`ah (Tawba) lakini haikuwa wazi ikiwa hilo lamaanisha kwamba Bismillahi ni aya katika kila sura ambazo wamethibitisha Bismillahi mwanzoni mwake, yaani Al-Faatiha na sura zilobakia isipokuwa Baraa`ah, au kwamba hiyo (Bismillahi) ni ya kupambanua baina ya sura na sura nyengine. Hivyo basi kukapatikana ikhtilaafu kati ya wanazuoni kuhusu kuwa Bismillahi ni aya katika Al-Faatiha, na kuwa ni aya katika sura zengine… lakini pamoja na hii ikhtilaaf wote wanakubali kwamba, Bismillahi imethibitishwa kimaandishi kwenye msahafu ambao maswahaba watukufu walikubaliana juu yake mwanzo wa Al-Faatiha na katika mwanzo wa sura zengine isipokuwa mwanzo wa Surah al-Baraa`ah, na hayo ni kwa makubaliano ya maswahaba radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote.

3- Imekuja katika kitabu cha As-Suyutwi (Al-Itqaan Fii Ulum al-Qur`an 1/234)

[Al-Faatiha: msimamo wa wengi ni aya saba, watu wa Kuffah na Makka wakahesabu Bismillahi bila ya kuhesabu أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ **“...ulio waneemesha”** [Al-Faatiha: 7] kuwa ni aya, na waliobaki ni kinyume. Na amesema Al-Hasan: ni aya nane, akazihesabu zote mbili kuwa aya. Na baadhi yao wamesema ina aya sita, hivyo hawakuzihesabu. na wengine wakasema ina aya tisa, wakazihesabu hizo pamoja na إِيَّاكَ نَعْبُدُ**. “Wewe tu tunakuabudu”** [Al-Faatiha: 5] (kuwa ni aya kivyake). Na inayotilia nguvu kauli ya kwanza ni hadith iliyopokewa na Ahmad, Abu Dawud, At-Tirmidhi, Ibn Khuzaima, Al-Hakim, Daaraqutniy na wengineo, kutoka kwa Ummu Salama kwamba Mtume (saw) alikuwa akisoma hivi:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ * الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ * الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ * مَالِكِ يَوْمِ الدِّينِ * إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ * اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ * صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلا الضَّالِّينَ

**KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU. Sifa njema zote ni za Mwenyeezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote; Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu; Mwenye kumiliki siku ya malipo. Wewe tu tunakuabudu, na wewe tu tunakuomba msaada. Tuongoe njia iliyonyooka. Njia ya ulio waneemesha, siyo ya walio kasirikiwa, wala walio potea.** [Al-Faatiha: 1-7] akazikata aya baada ya aya, na kuzihisabu kama wanavyohisabu mabedui. na akahisabu: بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ **“Kwa Jina la Mwenyeezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu”** kama aya, na hakuhisabu عَلَيْهِمْ**. “juu yao”** kuwa ni aya. Na amepokea Daaraqutniy kwa Sanad sahihi kutoka kwa Abd Khair akisema kwamba Ali aliulizwa kuhusu “Sab’ ul Mathaani” akajibu: ni الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ “Sifa njema zote ni za Mwenyeezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote” akaambiwa: lakini hiyo ina aya sita! akasema: بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ “Kwa Jina la Mwenyeezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu” ni aya] Mwisho wa Nukuu.

***Endelea... UK 11***

Na hii ina maana kwamba ikhtilaafu kuhusu maudhui ya Bismillahi kuwa aya…. n.k haya yanaingia katika mlango wa ijtihaad kwa dalili sahihi kwa wenye kujitahidi, na kuwafuata wanazuoni wenye kujitahidi na wanaozingatiwa, hilo ni jambo limo ndani ya sheria...

4- Na hakika yaliyooingizwa kwenye msahafu kama vile vitone, irabu, na kuwekwa alama za vikomo, na alama za hukmu za kusoma… n.k au yaliyowekwa mwishoni mwa baadhi ya misahafu kama dua, au yaliyoko pambizoni kama vile tafsiri na ufafanuzi… yote hayo hayaathiri katika Qur`an kuchanganyika na vitu vyengine. Kwani Waislamu wameihudumia Qur`an huduma kubwa, na mamilioni miongoni mwao wameihifadhi, na maandishi yake yamekuwa kwa mapokezi ya wengi kutoka kwa wengi, hivyo ikawa haitarajiwi kuwa itachanganyika na vitu vyengine na kuwatatiza watu. Kwa hiyo, ndio maana Waislamu tangu mamia ya miaka wameingiza kwenye misahafu baadhi ya mambo yanayosaidia kuisoma Qur`an kama vile vitone na irabu na vitu vyengine, na wala hayo hayakuathiri maandishi ya Qur`an tukufu… kwa hiyo basi, Dola ya Khilafah haitozuia uwepo wa hizi irabu na alama za vikomo… ndani ya misahafu.

Ufupisho ni kwamba, kutokea kwa ikhtilaafu katika ijtihaadi kuhusiana na Bismillahi kwamba ni aya katika Al-Faatiha au sio aya, au kwamba Al-Faatiha aya zake ni 6 au 7… au kwamba yasomwa kwa siri au kwa sauti… yote hayo hayaathiri katika hifadhi wa Mwenyezi Mungu kwa Qur`an tukufu, kwani, Bismillahi ni aya katika Surat al-Namli. Na Qur`an imekusanywa kwenye msahafu mmoja tangu zama za Makhalifa waongofu Mwenyezi Mungu awaridhie, kama ilivyoandikwa mbele ya Mtume (saw), na kama walivyoisoma kutoka kwa Mtume wa mwenyezi Mungu. Na amesema kweli Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa neno lake:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ **“Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda.”** [Al-Hijr: 9]

Natumai hayo yanatosheleza na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi na Mwenye hekima zaidi.

Ndugu Yenu,

**Ataa Bin Khalil Abu Rashtah**

**26 Dhul Qa’adah 1443 H**

**25/6/2022 M**

**Wanaharakati wa Hizb ut Tahrir Kenya wakigawanya toleo juu ya mada "Chaguzi za Kidemokrasia ni Sarabi, Hudhaniwa ni Maji kwa Mwenye Kiu" baada ya swala ya Ijumaa tarehe 29 Julai 2022.**

